

KITONGOJI CHA UVINJE,
KIJIJI CHA SAADANI,
WILAYA YA BAGAMOYO,
MKOA WA PWANI,
TANZANIA.

7/10/2002

MWENYEKITI WA TUME YA
HAKI ZA BINAADAM NA UTAWALA BORA,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

**YAH: UNYANYASAJI HUU NI HAKI ZA BINADAMU NA
UTAWALA BORA NCHINI?**

Mheshimiwa, kwanza tunaomba radhi kwa tutakayoyasema hapa iwapo tunakosea. Lakini imebidi kufanya hivyo kwa kukosa mtetezi.

Nchi yetu inaheshimika sana ndani na nje ya mipaka yetu katika jitihada za kuwatendea haki za binaadam wote. Lakini heshima hii, inavurugwa na baadhi ya viongozi kwa matatizo na mitazamo yao binafsi au chuki dhahiri.

Baada ya serikali kututaka tuhame eneo letu la kitongoji cha asili yetu, ambapo ndipo tunapoweza kudumisha uhai sisi na vizazi vyetu, ili tuwapishe wageni wa kutalii na wanyamapori, tumegeuziwa kibao kingine cha chuki inayopelekea hata kukiukwa mipaka ya utu, sheria na katiba inayolinda raia na mali zao. Ikumbukwe kiumbe chochote uhai wake unategemea mazingira yanayomzunguka pale alipo.

Mara baada ya mijadala hiyo kukwama mwaka 2001, mwaka 2002 tukaletewa vikosi vya askari wa wanyama toka ndani na nje ya hifadhi ya Saadani, hapa kitongojini. Tukavamiwa eti tunafanya ujangili uliokithiri. Tumepekuliwa bila ya vibali ndani na nje ya majumba yetu hakuna kilichopatikana.

Baada ya miezi 3 ya tukio hilo, tukavamiwa tena na Polisi toka Kibaha, Chalinze na Miono na kupekuliwa bila vibali eti sisi ni majambazi tunalima Bangi, tunakaba watu n.k. hakuna kilichopatikana. Hadi leo hatukujulishwa chochote.

Wenyewe tumejijenga sana kwa vitega uchumi vinavyotufanya tuweze kumudu maisha yetu hapa. Japo serikali imetutupa mkono kutulinda sisi na mazao yetu yanayomalizwa na wanyama yote tumevumilia.

Tunaomba kamati yako ilione hili na kulipatia jibu kwani maisha yetu sasa ni wasiwasi kila kukicha.

Wasalaamu.

Nakala:

- WAZIRI MKUU
- WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII
- WAZIRI WA MAMBO YA NDANI
- MBUNGE WA CHALINZE
- MKUU WA MKOA PWANI
- MKUU WA WILAYA BAGAMOYO

UVINJE SUB-VILLAGE
SAADANI VILLAGE
BAGAMOYO DISTRICT COAST REGION

TANZANIA.

7/10/2002

CHAIRMAN

COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

DAR ES SALAAM

TANZANIA

RE: IS THIS OPPRESSION PART OF HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE IN THE COUNTRY?

Honourable, we apologize for the comments we are going to make below. We are forced to do that because we have nobody to come to our defence.

Our country is respected within and outside our borders for our human rights record. But this respect is being eroded by some leaders for their own benefit or sheer hatred.

After the gov't wanted us to vacate the area of our ancient village of origin, where we can dwell with our generations, so that we can pave way for tourists and wild animals, we have been given another face of hatred which has led to human rights abuse, law and the constitution which protects the citizens and their property. It should be remembered that any living thing depends on the environment surrounding it.

After those discussions stalled in 2001, in 2002 a contingent of game warders was brought in from within and outside of Saadani into this sub-village. We were invaded for alleged committing crime. We have been searched without search warrants inside and outside our homes only to find nothing.

Three months later, we were again invaded by police from Kibaha, Chalinze and Miono and searched without search warrants on grounds that we are criminals growing bhang, taking people (hostage) and so on. Nothing tangible was found. We have not been informed of anything till date.

We have strived economically to sustain ourselves here, despite the fact that the government has turned deaf ears on us to protect us and our farm produce which is mauled by wild animals. We have persevered all this.

We pray that your commission acts on this matter because we live in fear everyday.

Thank you!

CC:

- Prime Minister
- Minister for Natural Resources and Tourism
- Chalinze Member of Parliament
- Coast Regional Commissioner
- Bagamoyo District Commissioner